SHUGHULI ZA KISWAHILI - GRADE 4 END TERM 2 EXAMS 2023

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA
Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.



Neema : Salaam aleikum sahibu yangu.

Juhudi : *(Kwa furaha)* Aleikum salaam msena wangu. Wambaje ?

Neema : Sina la kuamba.

Juhudi : Mimi pia sina neno. Ninakuomba twende nyumbani kwetu kwa matembezi..

Neema : Nashukuru kwa makaribisho. Ningetaka kwanza niwapigie wazazi wangu simu niombe ruhusa. *(Anapiga simu)*

Juhudi : *(Akimtazama kwa makini)* Je, wamekupatia idhini?

Neema : (Kwa tabasamu) Naam! Lakini baba ameniambia ikifika saa kumi na moja jioni niwe nimerudi nyumbani.

(Wote wanatembea pamoja)